**SEHEMU YA KWANZA :LUGHA** ***Muda: Saa 1 Dakika 40***

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 50.
2. Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-
   *(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako*

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne.***

***Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Kuku ni ndege mmoja ____1___ faida sana____2___ maisha ya ____3___. Kuku____4___ binadamu mayai____5___. Mayai ____6___ yakiuzwa huleta pesa____7___ ____8___ humwezesha mzazi ____9___ chakula, kulipia____10___ ya shule,kununua ____11___ ya watoto na ____12___ kuwapelekea ____13___ kila wanapougua ____14___ wapate____15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. wenye | B. mwenye | C.yenye | D.zenye |
| 2. | A.katika | B.kuliko | C.kwa | D.ndani mwa |
| 3. | A.mwanadamu | B.mfugaji | C.binadamu | D.mtu |
| 4. | A.humpea | B.hupeana | C.hupatikana | D.humpa |
| 5. | A.meupe | B.nyeupe | C.jeupe | D.leupe |
| 6. | A.hizi | B.hili | C.haya | D.hawa |
| 7. | A.mingi | B.nyingi | C.wingi | D.mengi |
| 8. | A.ambazo | B.ambapo | C.ambako | D.ambamo |
| 9. | A.kununua | B.kununuliwa | C.kununulia | D.kununulisha |
| 10. | A.charo | B.kigaro | C.nauli | D.karo |
| 11. | A.mavazi | B.maleba | C.sare | D.fulana |
| 12. | A.pamoja | B.hata | C.wala | D.pasi |
| 13. | A.kituoni | B.hospitali | C.hospitalini | D.matibabu |
| 14. | A.hili | B.ila | C.labda | D.ili |
| 15. | A.kuaguliwa | B. kutiliwa | C.kudungwa | D.kupewa |

***Kuanzia swali la 16-30, jibu swali kulingana na maagizo.***

16. Chagua vazi lisilovaliwa shingoni

A. mkufu B. herini
C. kidani D. kikuba

17. Ni neno lipi halifai kuwa katika kikundi hiki?

A. tembe B. machela
C. sirinji D. mswaki


18. Shemu ya mkono ambayo huvishwa saa ni

A. kisugudi B. kisigino
C. kiwiko D. nyongo

19. NI ipi si zana ya vita

A. fito B. bastola
C. sime D. manowari

20. Jina la umbo hili ni



A. moyo B. kopa
C. mche D. utao

21. ***Ni sentensi gani iko katika wakati uliopo***

A. waliimba wakacheza
B. tutaenda kupiga mbizi
C. wangekuwa wamefurahi
D. ninatamani pilau

22. Ndungu wa kiume wa mama huitwa

A. shemeji B. mjomba
C. wifi D. shangazi

23. Maina alinunua kishazi cha

A. ndizi B. samaki
C. nyanya D. matunda

24. ***Kamilisha methali ifuatayo***
***Hakuna masika yasiyokuwa na***

A. mafuriko B. mbu
C. hasara D. mvua

25. ***Andika tarakimu ifuatayo kwa maneno 101,101***

A. Kumi elfu na moja mia moja na moja
B. Mia moja elfu na moja na mia moja
C. Laki moja na moja elfu mia moja na moja
D. Laki mia moja na moja elfu, na mia moja na moja

26. Mtu anayetengeneza vyombo kutokana na mbao huitwa

A. sonara B. mhunzi
C. mwashi D. seremala

27. Eleza maana ya istiara hii
***Wekesa ni swara***

A. anafanana na swara
B. ana mbio sana
C. hana tabia nzuri
D. ni kiguu na njia

28. Mvua ______ sana.

A. imenyesha B. umenyesha
C. limenyesha D. yamenyesha

29. ***Tumia kiashiria radidi kujaza pengo***
______***ndimo tunamoishi***

A. humo huko B. huku huku
C. kuko humu D. humu humu

30. Makao ya mfalme huitwa

A. kasri B. ikulu
C. bweni D. pango

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 31 - 40.***

Aliishi mzee mmoja aliyeitwa Ole Kapunda. Mzee huyu alikuwa na umri wa takribani miaka sabini. Kwa umbo hakuwa mnene wala mwembamba. Kilichowashangaza wengi ni ndevu zake zilizokuwa ndefu na hata kufikia magoti. Alipoketi ndevu zake ziligusa chini.

Macho nayo yalikuwa makubwa kweli kama gololi. Shabash! kucha zake nazo zilikuwa ndefu zenye urefu wa kama sentimita nane hivi nazo za miguu zilikuwa vivyo hivyo.

Mzee Kapunda alikuwa na wake wawili: Cheusi na Katunda. Cheusi alikuwa mweupe pe kama Mwingireza, naye Kutunda mweusi ti kama chungu cha kupikia. Wanawake hawa wawili hawakuwa na watoto; hivyo basi walikuwa tasa. Jambo la kufurahisha ni kuwa ***kiamboni*** mwa mzee Ole Kapunda kulikuwa na furaha kila wakati. Kazi za nyumbani walizigawanya kwa usawa.

Cheusi ndiye aliyemchana Kapunda nywele, naye Kutunda kumchana ndevu zilizokuwa na ***mvi***. Jioni walipumzika sebuleni iliyokuwa na kuta za udongo zilizopakwa rangi nyeupe. Mle ndani waliwasha moto wa kuwapasha joto na kuwapa mwangaza. Kumbuka wakati huo hakukuwa na taa. Hata kwenda usiku watu walitumia vijinga. Fikiria kulikuwaje wakati huo!

---

**31.** Idadi ya miaka aliyokuwa naye mzee Kapunda ilikuwa

A. sitini B. sabini
C. hamsini D. thelathini

**32.** Sifa zilizotajwa kwenye hadithi ambazo mzee huyu alikuwa nazo ni ngapi?

A. Moja B. Tatu
C. Mbili D. Nne

**33.** Kati ya wake wa mzee Kapunda ni nani aliyekuwa mweusi?

A. Kutunda B. Cheusi
C. Kapunda D. Ole

**34.** Kisawe cha neno ***kiamboni*** kama lilivyotumika katika habari hii ni

A. shambani B. malishoni
C. ugani D. nyumbani

**35.** Ni kweli usiopingika kusema

A. Mzee Ole Kapunda alikuwa na umri wa miaka sabini
B. Mzee Ole Kapunda hakuwa na ndevu ndefu
C. Kutunda na Cheusi hawakuwa tasa
D. Cheusi alikuwa mweusi ti.

**36.** Ni sentensi ipi ambayo haimwelezi mzee Kapunda?

A. Alikuwa na kucha ndefu za miguu na mkono
B. Alikuwa mrefu kama mlingoti
C. Alikuwa na macho makubwa
D. Alikuwa na umbo la wastani

**37.** Neno ***shabash!*** litatiwa katika kipengele kipi katika lugha?

A. kiashiria B. mshangao
C. nomino D. kivumishi

**38.** Maana ya neno ***'mvi'*** ni

A. Nywele za kipilipili
B. Nywele za kitimtim
C. Nywele za kijivu
D. Nywele za sharafa

**39.** Kati ya wanawake hawa wawili ni nani aliyemtayarisha Kapunda chakula?

A. Ole B. Cheusi
C. Kutunda D. Hatukuelezwa

**40.** Raha kiamboni mwa mzee Kapunda ililetwa na

A. Kutunda na mumewe
B. Bwanake Cheusi na majirani
C. Ukosefu wa wana katika nyumba hiyo
D. usikilizano ulioletwa na kiongozi

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 41 - 50.***

Wananchi wa leo na vizazi vijavyo, maisha ya maendeleo yao yanategemea maliasili ya nchi ambayo ni rasilimali kama vile misitu, wanyamapori, mito, maziwa na maeneo kinamasi. Rasilimali hizi ni muhimu kwa utoaji wa huduma kiuchumi na kijamii. Kwa hiyo kumaliza rasilimali hizo ni kuharibu mazingira endelevu ya shughuli za kiuchumi.

Kwenye upande wa misitu, Kenya imebarikiwa kuwa na hekari elfu themanini za nyika na misitu. Misitu hiyo inajumuisha ile iliyopandwa katika hifadhi ya wanyama, vyanzo vya maji, ufugaji nyuki na dawa asili.

Msitu wa Mau umekumbwa na matatizo chungu nzima. Hayo ni pamoja na ukataji miti ovyo, huduma duni ya ugani, viwanda vya mbao, uwindaji haramu na uchomaji wa makaa. Msitu huu ni hifadhi ya mvua na maji katika taifa la Kenya. Uwindaji haramu unatishia uhai wa viumbe vingi msituni.

Wizara za mazingira na utalii zinajitahidi kulinda vivutio vyetu kwa manufaa ya kizazi cha kesho. Kuna mimea kama vile milengalenga,mikoko, misonobari na mikalitusi kwenye msitu huu. Hatufai kuichoma misitu kwa sababu hali ya mvua na mazao itapungua nao wenzetu watakufa njaa. Ni lazima kama ibada kwetu kuwajibika kuilinda misitu yetu. Chambilecho wahenga 'usipoziba ufa, utajenga ukuta'?

**41.** Maendeleo ya vizazi vya kesho yatategemea nini?

A. Maliasili  B. chakula
C. kusoma kwa bidii  D. mazingira yao

**42.** Wanyamapori, maziwa, mito na misitu kwa jumla huitwa

A. wanyama  B. mifugo
C. maliasili  D. rasilimali

**43.** Taifa la Kenya lina hekari ngapi za nyika na misitu kwa nambari?

A. 30,000  B. 80,000
C. 8,000  D. 38,000

**44.** Ni tatizo lipi halijaukumba msitu wa mau?

A. Ukataji ovyo wa miti
B. Uwindaji haramu wa wanyama
C. Ukosefu wa viwanda vya mbao
D. Huduma duni ya ugani

**45.** Unapowawinda wanyama msituni, matokeo huwa yapi?

A. Mvua hupotea
B. Utalii utaendelea kuwa imara na bora
C. Misitu yote itafungwa na maji mengi yatapotea
D. Uhai wa viumbe utakosekana

**46.** Ni wizara ngapi zimetajwa katika ufahamu uliosoma?

A. Mbili  B. Elfu themanini
C. Kumi  D. Tano

**47.** ***'Usipoziba ufa utajenga ukuta'***

Hii ni fani gani ya lugha?

A. msemo  B. kitendawili
C. methali  D. tashbihi

**48.** Msimamizi wa wizara yoyote katika nchi huitwa?

A. Rais  B. Waziri
C. Katibu mkuu  D. Balo

**49.** Ni kipi kati ya hivi si kivutio cha nchi kulingana na maoni yako?

A. Hifadhi  B. Muga
C. Chemchemi  D. Uwindaji

**50.** Taja jina jingine lenye maana sawa na msitu

A. kusaka  B. pori
C. kichaka  D. talanta